UK 7

# Maadhimisho Siku ya Chakula Duniani kufanyika kitaifa Njombe

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

SERIKALI imesema maadhimisho ya siku ya chakula duniani yatafayika kitaifa mkoani Njombe ambapo yanalenga kuhamasisha jamii kuwa na uhakika wa chaula na lishe bora.

Kauli hiyo ya serikali ilitolewa jana na Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jijini Dodoma na kueleza kuwa maandalizi yamekamilika.

"Kwa wakazi wa Mkoa wa Njombe na mikoa jirani ya Nyanda za Juu Kusini, nawaomba mjitokeze kwa wingi kwenye maadhimisho ambayo yatazinduliwa rasmi kitaifa Oktoba 10 mwaka huu na kufikia kilele chake Oktoba 16 mwaka huu mkoani Njombe," alisema Mgumba.

Naibu Waziri huyo aliongeza kuwa, kila mwaka makao makuu ya Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) huzitaka nchi wanachama kuhamasisha wadau wote wa Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kuchangia katika kuhakikisha kila mtu anawezeshwa kupata chakula bora na cha kutosha wakati wote wa maisha yake.

Alibainisha kauli mbiu ya maadhimisho ya mwaka huu inasema î Kesho Njema Inajengwa na Lishe Bora Endelevuî ambapo ameliipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuitekeleza kwa vitendo kauli mbiu hiyo upande wa uzalishaji mazao ya chakula.

"Tathmini iliyofanyika hivi karibuni ya uzalishaji kwa msimu wa 2019/2020, inaonesha kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula unatarajia kufikia tani 17,742,388 ambapo mahitaji ni tani 14,347,955. Mahitaji haya yakilinganishwa na uzalishaji nchi inategemewa kuwa na ziada ya tani 3,511,620 za chakula ambapo tani 1,322,020 ni za mazao ya nafaka na tani 2,072,413 ni za mazao yasiyo nafaka," alisitiza Naibu Waziri Mgumba.

Kuhusu tatizo la lishe bora linalopelekea udumavu, Naibu Waziri Mgumba alisema, takwimu zinaonesha kuwa udumavu umepungua kutoka asilimia 42 mwaka 2010 hadi asilimia 32 mwaka 2018 na ukondefu umepungua kutoka asilimia 3.8 mwaka 2014 hadi asilimia 3.5 mwaka 2018 ambayo ni chini ya kiwango cha malengo ya Mkutano wa Afya Duniani (WHA) cha asilimia 5.



> *Kwa wakazi wa Mkoa wa Njombe na mikoa jirani ya Nyanda za Juu Kusini, nawaomba mjitokeze kwa wingi kwenye maadhimisho ambayo yatazinduliwa rasmi kitaifa Oktoba 10 mwaka huu na kufikia kilele chake Oktoba 16 mwaka huu mkoani Njombe ...*
>
> **Omary Mgumba**
> Naibu Waziri wa Kilimo

Mgumba alitaja mikoa inayozalisha chakula kwa wingi ndiyo yenye viwango vikubwa vya udumavu kwa watoto kwa mfano Njombe ina udumavu wa asilimia 53.6 wakati uzalishaji mazao ni tani 446,491 kuwa na kiwango cha utoshelevu-SSR asilimia 194 na mkoa wa Rukwa asilimia 47.9, huku uzalishaji ni tani 943,002 na kiwango cha Utoshelevu-SSR asilimia 230.

Iringa ina udumavu wa asilimia 47.1, huku uzalishaji ni tani 470,750 na kiwango cha utoshelevu-SSR asilimia 161 na Songwe ina udumavu asilimia 43.3 huku uzalishaji mazao ni tani 805,545 na kiwango cha utoshelevu cha asilimia 210.

Naibu Waziri Mgumba alisema, hali hii ya udumavu ndio imepelekea Wizara ya Kilimo na wadau kukutana mkoani Njombe pamoja na kuhamasisha uzalishaji mazao ya chakula elimu ya lishe bora kutoka kwa wataalam itatolewa katika siku zote saba ikiwemo uhamasishaji ulaji vyakula vya asili yenye protini nyingi.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo ,Gerald Kusaya alisema kamati ya maadalizi ya maadhimisho hayo ngazi ya taifa na ile ya mkoa wa Njombe zimefanya kazi nzuri kuhamasisha wadau zikiwemo taasisi za umma na binafsi kujitokeza kushiriki.

Kusaya alisema, Wizara ya Kilimo inaendelea kutoa wito kwa wadau zaidi kujitokeza kwenye maadhimisho ya mwaka huu na kuwa yanalenga kuwawezesha wakulima na wananchi kujua kanuni bora za uzalishaji mazao ya chakula,uhifadhi,teknolojia ya uongezaji thamani na elimu ya masuala ya lishe bora.

"Tunawashukuru wadau wetu FAO,WFP,UNICEF. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, BRITEN, Licolto, Wizara ya Mifugo na Uvuvi,Wizara ya Afya kwa ushrikiano wao kwa Wizara ya Kilimo kuandaa maadhimisho ya mwaka huu," alisema Kusaya.

Maadhimisho ya mwaka huu ni ya 40 tangu yalipoanza kuadhimishwa mwaka 1945 na Shirika la Chakula na Kilimo la Umaoja wa Mataifa (FAO).Maadhimisho ya siku ya chakula mwaka uliopita yalifanyika mkoani Singida.

Scanned with CamScanner

# Wadau watumia Sh bil 29 kununua maziwa

Na UPENDO MOSHA
- MOSHI

WADAU wa maziwa nchini wametumia Sh bilioni 19,2 kununua maziwa, ikiwa ni sehemu ya mchango wa kuhamasisha unywaji wa maziwa shuleni hatua ambayo itasaidia kukuza uchumi na upatikanaji wa masoko kwa vyama vya ushirika vya maziwa.

Fedha hizo ambazo zimetumika mwaka 2016 hadi 2020, zimedaiwa kunufaisha shule 210 za msingi na sekobdari, huku zaidi ya lita milioni 12 zikisambazwa katika shule hizo kwa wanafunzi.

Akizungumza mjini hapa jana, wakati wa maadhimisho ya siku ya unywaji Maziwa shuleni duniani ambayo kitaifa imefanyika mkoani Kilimanjaro, Kaimu Msajili wa Bodi ya Maziwa Tanzania, Noel Byamungu, alisema mpango huo ni endelevu na unategemewa kuwa na manufaa makubwa.

"Shilingi bilioni 19.2 zimetumika kununulia bidhaa za maziwa kwa ajili ya mpango wa unywaji wa maziwa mashuleni, utachangia katika kukuza uchumi kwa wazalishaji pamoja na upatikanaji wa masoko ya uhakika," alisema Byamungu.

Alisema shule 30 bado ziko kwenye mpango wa unywaji wa maziwa, kati ya hizo 24 zipo Kilimanjaro.

Mkurugenzi wa Usajili na Masoko wa Bodi ya Maziwa, Stephen Michael alisema kuna viwanda 99 vya usindikaji wa maziwa ambavyo vina uwezo wa kusindika maziwa lita 865,600 kwa siku.

Alisema licha ya viwanda hivyo kuwa na uwezo huo, vimekuwa vikisindika lita 203,600 kwa siku, ni sawa na asilimia 23.52 kutokana na changamoto kubwa ya ukosefu wa malighafi jambo ambalo limekuwa likiendelea kuzorotesha ukuwajinwa sekta hiyo.

"Kati ya viwanda 99, viwanda nane havina uwezo wa usindikaji, sekta hii imekuwa ikikabiliwa na changamoto nyingi, ikiwemo ukosefu wa malighafi lakini pia kumekuwa na tija ndogo ya uzalishaji wa maziwa kutokana na kuwepo na malisho duni kwa mifugo hivyo kukosekana kwa wingi wa maziwa," alisema Michael.

Alisema Tanzania ni ya pili duniani kwa wingi wa mifugo na uzalishaji upo chini ikilinganishwa na mifugo iliyopo ambapo mwaka jana ng'ombe walikuwa milioni 33.4 ambao wamezalisha maziwa lita bilioni 3.01.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, alisema mpango wa unywaji wa maziwa mashuleni utasaidia kukuza uchumi uzalishaji pamoja na wauzaji wa maziwa kupata masoko.

Scanned with CamScanner

# Serikali kufufua Tafico

Na FARAJA MASINDE
- DAR ES SALAAM

SERIKALI imejipanga kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO), lengo likiwa ni kuongeza uchumi wa viwanda.

Pia imesema katika jitihada za kutafuta vyanzo vya fedha kwa ajili ya kufufua shirika hilo, Serikali ya Japani imefadhili Sh bilioni 4.2 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na ununuzi wa meli.

Akizungumza Dar es Salaam jana,wakati wa kikao cha kujadili namna gani vifaa vya TAFICO vitakavyonunuliwa, Mkurugenzi Idara ya Uvuvi Tanzania Bara, Magese Bulai kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuv,i Dk. Rashid Tamatamah alisema , TAFICO pekee ndiyo iliyokuwa dira ya kuchangia uchumi wa uvuvi toka mwaka 1974.

Alisema shirika lilitakiwa kubinafsishwa lakini halikubinafsishwa kwa kuwa hakutokea mwekezaji hadi mwak 2015 Serikali ilipoamua kulirudisha mkononi mwake.

Alisema kabla ya kubinafshishwa, Serikali ilitoa tangazo kuwa yeyote atakayetaka kuwa mwekezaji wa shirika hilo anatakiwa asibadilishe matumizi ya shirika hilo .

Alisema hivi sasa wapo katika hatua nzuri kwa ajili ya kufufua shirika hilo kwa kuwa baadhi ya mali zisizoamishika bado zipo mkononi mwa shirika hilo.

Alisema hadi sasa Mkoa wa Dar es Salaam kuna mali zisizoamishika zenye thamani ya Sh bilioni 118.6, huku mikoa mingine ikiwa na mali za aina hizo.

Kaimu Meneja Mkuu wa TAFICO, Esther Mulyila alisema katika awamu hii ya tano wanataka ifanye shughuli zake katika bahari kuu ili kuzalisha sekta ya uvuvi.

“Serikali inajua umuhimu wa kuwepo kwa TAFICO kwa kuwa inachangia pato la uvuvi na kuwapatia vijana wengi ajira.

“Pia ukiangali Tanzania bado yhainufaiki na bahari kuu badala yake imekuwa ikitoa tu vibali kwa meli za kigeni, hivyo mkakati wa sasa ni kuona Tanzania ikinufaika na bahari kuu ndiyo maana tunaweka mikakati,”alisema.

Alisema kufufuliwa kwa shirika hilo, ni moja ya kuongezeka kwa chanzo cha mapato nchini hivyo watahakikisha shirika hilo linapata meli za kutosha kwa ajili ya uzalishaji mali.

Scanned with CamScanner

MTANZANIA UK 10

JULIAN SANGA



AHADI

# Mgombea atoa ahadi kujenga kiwanda cha maziwa

Na SAFINA SARWATT - MWANGA

**MGOMBEA** ubunge Jimbo la Mwanga mkoani Kilimanjaro, Joseph Tadayo (CCM), amewahakikishia wananchi wa Kijiji cha Songoa kata Ngujini atakwenda kuwashawishi wawekazaji kutoka nje ya nchi na ndani kuwekeza kiwanda cha kusindika maziwa ili kuongeza mapato kama atachaguliwa.

Alisema kijiji hicho kinaongoza kwa uzalishaji wa maziwa, lakini changamoto kubwa soko la uhakika hali inayowalazimu wananchi kuuza kwa bei ndogo.

Tadayo aliyasema hayo jana, wakati wa mkutano wa kampeni uliofanyika Kijiji cha Songoa.

Alisema endapo atachaguliwa kuwa mbunge,atahakikisha anawainua kiuchumi kwa kuimarisha ushirika wa mazao mbali mbali ya chakula na biashara ,ufugaji,utafutaji wa masoko kilimo na upatikanaji wa maji safi na salama.

"Mbali na ilani ya chama changu, nimefanya utafiti na kutambua kero mbali mbali za wakazi wa mwanga ikiwemo utatuzi wa kero kubwa ya upatikanaji soko la maziwa nitakwenda kuhamasisha wawekezaji kuja kuwekeza katika kiwanda cha kusindika maziwa,"alisema.

Alisema uwekezaji wa kiwanda cha maziwa itachochea na kuboresha maisha ya wafugaji wa ng'ombe na kufuga kisasa.

Aliahidi kupambana na kero ya upatikanaji wa maji, ubovu wa miundombinu za barabara unamalizika ndani ya wilaya ya mwanga.

"Nitahakikisha kunakuwapo na shule zenye kidato cha tano na sita na kukarabati shule ya sekondari pamoja na kujenga vyoo vya wanafunzi na walimu,"alisema.

"Ndugu zangu wananchi wa mwanga Oktoba 28 mnichague kuwa mbunge wenu pamoja na mgombea Rais wa CCM ,Dk.John Magufuli ili tuweze kushirikiana na katika kuongeza vyumba vya maabara kwa ajili ya masomo ya vitendo ya sayansi na komputa,"alisema

Alisema vituo vya afya atahakikisha vinapatiwa madawa ya kutosha na wataalamu wa afya ili wananchi waweze kupata huduma za afya karibu na makazi yao.

Alisema pia atatumia nafasi hiyo kuwafundisha wakulima na wafugaji namna ya kuongeza thamani ya mazao yao na kuwatafutia masoko ya mazao kitaifa na kimataifa ili kuwakwamua na umasikini.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi alisema Serikali imejipanga kujenga hospitali ya wilaya ya mwanga itokayoweza kutoa huduma zote za afya ikiwemo huduma ya upasuaji.

Alisema imetoa Sh milioni 400 za ujenzi wa kituo cha afya Usangi na imetumia zaidi ya Sh milioni 955 kwa ajili ya ununuzi wa dawa katika zahanati na vituo vya afya.

Scanned with CamScanner

Baltazar Mashaka)

UHURU UK5

# *Mapato ya uvuvi yaongezeka Kagera*

**Bukoba**
**NA ALODIA BABARA**

MAPATO yanayotokana na uvuvi yameongezeka mkoani Kagera kutoka sh. milioni 891.6 mwaka 2014/2015 hadi kufikia sh. bilioni 3.06 zilizokusanywa mwaka 2019/2020.

Akiongea na gazeti hili jana, Ofisa Uvuvi Mkoa wa Kagera, Efrazi Mkama, alisema mapato yanayotokana na uvuvi yameongezeka kutoka sh. milioni 891.6 na kufikia sh. bilioni tatu ambayo ni sawa na asilimia 133.2 ya malengo yaliyowekwa ya sh. bilioni 2.3 kwa mwaka.

Mkama alisema katika makusanyo hayo Halmashauri ya Wilaya ya Muleba ilivuka lengo lililowekwa kwa kukusanya asilimia 144.9, Karagwe 289.9, Biharamlo 220.0 na Misenyi 168.4 ya lengo lililowekwa.

Alieleza kwamba jumla ya tani 7,266 za sangara zilivunwa mkoani hapa kwa mwaka 2020 zenye thamani ya sh. bilioni 42.15.

" Nguvu ya uvuvi ziwani imeongezeka ambapo mwaka huu wamefikia wavuvi 23,878 na mwaka 2000 walikuwa wavuvi 9,616,"alisema Mkama.

Alieleza kwamba idadi ya mitumbwi imeongezeka kutoka 3,395 mwaka 2015 hadi mitumbwi 4,108 mwaka 2020.

Serikali ya mkoa huo imeendelea kulinda ubora wa mazao ya samaki ambapo idadi ya ukaguzi imeongezeka kutoka 96 mwaka 2015 hadi ukaguzi 166 mwaka 2019/2020 katika mialo, masoko, maghala na viwanda vya samaki matokeo ya ukaguzi yalionyesha kukidhi viwango vya ubora vya kitaifa na kimataifa.

Scanned with CamScanner

...ulidai, alimwona mkewe akiwafungulia mlango na wakaingia

UHURU UK 21

# Serikali yaingia makubaliano na Japan kuifufua TAFICO

**Mkuranga**

**NA REHEMA MAIGALA**

SERIKALI ya awamu ya tano katika kuendeleza sekta ya uvuvi nchini, imejipanga kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania TAFICO, lengo likiwa ni kuongeza chachu ya maendeleo katika kukuza uchumi wa viwanda.

Katika kufanikisha hilo, serikali imeingia makubaliano na Japan, ambapo zaidi ya sh. bilioni 4.2 zitatolewa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na meli kubwa ya uvuvi.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, katika kikao cha majadili kuhusu ununuzi wa vifaa hivyo, Mkurugenzi Idara ya Uvuvi Tanzania Bara, Magese Bulai, kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Dk. Rashid Tamatamah, alisema kufufuliwa kwa Shirika hilo ni neema kwa wavuvi.

Alisema TAFICO pekee ndio iliyokuwa dira ya kuchangia uchumi wa uvuvi tangu mwaka 1974, hivyo kutokufanya kazi kwake kumepunguza mapato.

"Shirika hilo lilitakiwa kubinafsishwa, lakini haikuwezekana badala yake, kwa kuwa hakukuwa na mwekezaji hadi mwaka 2015. Serikali ilipoamua kurudisha mikononi mwake,"alisema.

Alieleza kuwa wawekezaji wengi walishindwa masharti kwa kuwa serikali ilitaka kutokubadilisha matumizi ya shirika hilo.

Bulai, alisema hivi sasa wapo katika hatua nzuri kwa ajili ya kufufua shirika hilo kwa kuwa baadhi ya mali zisizoamishika bado zipo mkononi mwa shirika hilo.

Alisema hadi sasa katika Mkoa wa Dar es Salaam, kuna mali zisizoamishika zenye thamani ya zaidi ya sh.bilioni 118.6 huku mikoa mingine ikiwa na mali zaidi.

Naye Kaimu Meneja Mkuu wa TAFICO, Ester Mulyila, alisema katika awamu ya tano ya uongozi wa Rais Dk. Magufuli, ipo haja shirika hilo kufanya kazi ipasavyo ili kuboresha sekta ya uvuvi iweze kufikia malengo.

"Serikali inajua umuhimu wa kuwepo kwa TAFICO kwa kuwa inachangia pato la uvuvi na kuwapatia vijana wengi ajira, katika kukuza uchumi na maendeleo ya viwanda,"alisema Ester.

W
ita
ya
Lo
Vit
M
ut
as
M

Scanned with CamScanner